Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Shairi

Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain

Bismillah nitajayo, Ni jina la Mola wangu,
Rahmani isemwavyo, Ya akhera na ulimwengu,
Rahimi isimuliwavyo, Akhera ya wacha Mungu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Alhamdu ni sifa za Mola, Lillahi jina la Hadhiya,
Namwalia Rasula, Salaam na neema pia,
Waalaalihi liula, Zienee kwa wote pia,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Baada ya kumaliza, Sasa natunga shairi,
Naanza kujituliza, Nitaje kisa na maamuri,
Kidogo nitatambaza, Si sababu ya kujitafakhari,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ilahi kamtuma Rasuli, Muhammadi Liamini,
Awe mtetezi kamili, Aidhihirishe dini,
Nae kakubali, Kuwa kiongozi wa dini,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Kisa ninachoeleza, Maendeleo yaamini,
Agizo alitimiza, Alimtuma Manani,
Hakuna la kumtatiza, Mwislamu moyoni,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Wakati wa maisha yake, Muhammadi Rasuli,
Alimzaa mtoto mke, Fatimati Libatuli,
Kamuoza binami yake, Imamu Sayyidna Ali,

Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Mola mjuwa falagha, Ali akamzaa Husain,
Mwenyezi Mungu Kawapanga, Wajukuu zake amini,
Dunia ikawa na mwanga, Wakafurahi Malaika mbinguni,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Siku nyingi zikapita, Mustafa akatawafu,
Ndipo kuanza matata, Shamu mambo machafu,
Nakuzitangaza vita, Kuazimu ushupavu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Dini ikavurugwa, Kwa vitendo vya Yazidi,
Amani zikapotea, Maasi yakazidi,
Kidogo wafuatao njia, Ya Nabii Muhammadi,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikawa nyakati hizo, Zikapunguka imani,
Ikakithiri michezo, ya hali ya kishaitwani,
Wachache wafuatao nguzo, Nakuthibiti imani,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Na hali hapo zamani, Nabii alitamka,
Ya Husain minni, Wa–ana ilaika,
Ndipo kasimama Husain, Na amri akazishika,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Haki ikasimama, Na batili zikaondoka,
Mpaka siku ya Kiyama, Dini zitabadilika,
Fahimma hata Fahhama, Uislamu utatajika,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Na kifo chake kwa kamili, Ni fidia ya Uislamu,
Mfano wa Ismaili, Kwa Nabii Ibrahima,
Dini leo ni kamili, Imesimama salama,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Imamu aliposikia, Ilivyobadilika Shamu,
Aamuruvyo bini Muawiya, Mambo mengi ya haramu,
Na dini imepotea, Anadai na Uimamu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Imamu moyo ukasita, Akifikiri tarafa,
Yazidu anazozipita, Bila ya amali nadhifu,
Akasema haihata, Ila nende zangu Kufa,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Tarekhe ishirini na Nane, Akaondoka Madina,
Kwenda kulitufu Kaaba, Sharia iliyo bayana,
Yazidi Kakutubu kitaba, Kujisainisha laana,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Barua ya kutoka Shamu, Ikafika mjini Makka,
Kaarifiwa hakimu, Husain muuwe haraka,
Husain alipofahamu, Ikambidi kuondoka,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Imamu Husain ashirafu, Baada hayo kufahamu,
Akasema Makka ni tukufu, Kutia damu haramu,
Hicho ni kitendo dhaifu, Kakataza Rabi Karimu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikawa tarehe pili, Ya mwezi wa mfunguo nane,
Karbala akawasili, Kiasi cha saa nane,
Majeshi ya wakatili, Yakazuia maji wasinywe,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Mpaka tarehe saba, Mtoni kuna hatari,
Maadui wameziba, Na maneno ya jeuri,
Maji heri kunywa simba, Nguruwe na makafiri,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Islamu Kataharaki, Kooni kulikauka,
Kila akiwalahiki, Maji yao kuwataka,
Wao kuzidi hamaki, Huruma imewatoka,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Mama mtoto taabani, Maziwa yamekauka,
Hamna tone kifuani, Mtoto anahangaika,
Kayabisika midomoni, Damu zinamdondoka,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Wamezuia hayo maji, Watu elfu tano,
Wengi mno walindaji, Wa mishale bila mifano,

Ingawa anawahitaji, Wala hawana mapatano,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikipika siku tatu, Tangu waponyimwa maji,
Wameshikana hao watu, Kwa hali ya uziwiyaji,
Wakaona hiyana si kitu, Wana nia ya uuwaji,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Tarehe tisa ilipofika, Walitaka waanze vita,
Imamu Husain aliwataka, Ruhusa ya swala kupata,
Amuabudu Rabuka, Bila kumfika matata,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Mkuu wa jeshi la Yazidi, Ana moyo mughaladha,
Omar bini Saadi, Ameajiriwa kwa fedha,
Akishatimiza ahadi, Hataki kwa Mungu Karadha,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Asubuhi tarehe kumi, Vita ikaumuka,
Ndipo kuanza uvumi, Mishale kuipachika,
Omari mtaka dami, Mshale ukamtoka,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ndiye mwamrishaji, Vita kuamrisha,
Hakuna tena mkaaji, Muda wao umekwisha,
Hakuna tena kuhoji hoji, Kawamalizeni maisha,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikawa hekaheka, Hali ya vita ni kali,
Islamu kateseka, Maji yamewawiya mbali,
Mradi wana mashaka, Hawanywi wala hawali,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Alipofika mkatili, Mlaanifu mwingi wa balaa,
Na kisu chake kikali, Yuna kwitwa Shimr,
Imam aliomba aswali, Hakupenda amalize swala,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Alipotaka amuuwe, Alitamka Imamu,
Ebu nikuchungue, Nikujue mjirimu,
Akaona uso wa Nguruwe, Mara alimfahamu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Aliambiwa zamani, Uhai wa babu yake,
Atayemuua Husain, Atabadilika sura yake,
Awe mnyama wa mwituni, Nguruwe kwa jina lake,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Ikaja nyingi tufani, Ikatokea kusini,
Jua likazama mbinguni, Kukawa giza adhimu,
Ikashuka mvua mbinguni, Maji mekundu ya damu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Wakati walipomchinja, Adui walifurahi,
Mwili na waliuacha, Ili aponde ngamia,
Na mtoto wakamchinja, Bila ya kumhurumia,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Wanawake wakachojoa, Shungi zao za kichwani,
Huku wakiwasumbua, Wakatembezwa uraiani,
Kwa ukatili wa kuuwa, Ataulipiza Manani,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Kile kichwa ikabidi, Kama si kichwa cha mtu,
Kikapelekewa Yazidi, Akikanyage kwa Fimbo,
Fikra za mkaidi, Si kama fikra za utu,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Yazidi aliona vema, Hajui ameangamia,
Ndani ya Jahanama, Ndiko alikoingia,
Na maji yaja hima, Ndiyo anaumiya,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Hapa ninahitimu, Shairi nimekomesha,
Ingawaje nina hamu, Yakutaka kuzidisha,
Rabbi unirehemu, Kwa haya yangu maisha,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Na kila msikiaji, Mwenye roho ya mahaba,
Rabi mwondolee balaji, Mpokelee kila toba,
Yarabi utufariji, Kwa baraka ya Habiba,
Salaam Salaam, Imamu Sayyidna Husain.

Muienuddin Chishti Ajmeri Asema:

Shah ast Husain Badshah ast Husain
Din ast Husain Din Panah ast Husain
Sar daad, Na daad dast dar daste Yazid
Haqqa ke Binae Lailah ast Husain.

Maana yake:

Husain ni Mfalme (ni Bwana)
Husain ni Mfalme wa Wafalme (ni Bwana wa Mabwana)
Husain ni Dini, Husain ndiye mhifadhi wa Dini
kichwa alikitoa, bali hakutoa mkono wake kwaYazid
Hakika Husain ndiye msingi wa Lailaha illallah.

Source URL: https://www.al-islam.org/ar/node/40646#comment-0